

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA MWANZA

Telegram: "ADMIN"
Simu Na.:028 - 2590039 & 2590047
Fax.No. 028-2590203



OFISI YA MKUU WA WILAYA,
S .L .P. 89,
SENGEREMA

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na.CA.70/218/02/2

13 Februari, 2018

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI TAREHE 13 FEBRUARI 2018
UZINDUZI WA ZOEZI LA UPULIZIAJI DAWA YA UKOKO
MAJUMBANI MKOA WA MWANZA 2018

Ndugu Wananchi, napenda kutoa taarifa ya uzinduzi wa zoezi la upulizaji wa Dawa ya Ukoko ya kuuu mbu majumbani na malengo ya utekelezaji wa zoezi hilo kwa mwaka 2018 kwa Mkoa wetu wa Mwanza.

Ndugu Wananchi, Mkoa wetu wa Mwanza ni kati ya Mikoa yenye maambukizi ya ugonjwa wa malaria. Kwa miaka ya nyuma tumeshuhudia milipuko ya ugonjwa wa Malaria ambayo iliambatana na vifo hasa kwa watoto wenye umri chini ya miaka 5 na Mama wajawazito. Takwimu za malaria za mwaka 2016 zinaonyesha maambukizi ya malaria katika Halmashauri zetu tatu ni kama ifuatavyo Sengerema asilimia 10.1, Buchosa asilimia 12.7 na Kwimba asilimia 11.4.

Ndugu Wananchi, Kiwango hiki cha maambukizi kimekuwa kikipungua kutokana na utekelezaji wa mikakati mbalimbali ukiwemo huu wa upulizaji dawa ya ukoko majumbani ili kuuu mbu waenezao malaria.

Mkakati huu wa kupulizaji dawa ya ukoko majumbani unatekelezwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia Wazee na Watoto kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali la Abt Associates chini ya ufandhili wa Serikali ya Marekani, kupitia USAID. Utekelezaji wa mkakati huu unagharama kubwa lakini unamotokeo mazuri naya haraka endapo utatekelezwa kwa usahihi.

Ndugu Wananchi, Kwa mwaka 2017, unyunyiziaji ulifanyika katika Halmashauri ya Buchosa, Sengerema na Kwimba na jumla ya nyumba 184,559 zililengwa kupuliziwa. Kwa mwaka huu zoezi hili linategemea kuanza kesho tarehe 14/02/2018 katika Halmashauri zote tatu. Jumla ya nyumba 223,905 zimelengwa kupuliziwa.

Ndugu Wananchi, Kazi hii ya upuliziaji inafanywa na Wananchi wa maeneo husika ambao wamechaguliwa kutokana na sifa zao kulingana na kada husika, jumla yao ni 1,299. Zoezi hili litahusisha moja kwa moja wenyeviti wa Vitongoji wapatao 1,703. Hivyo basi, pamoja na vita dhidi ya malaria, zoezi hili linatoa ajira za muda na kuongeza kipato cha kaya kwa wale waliobahatika kushiriki.

Ndugu Wananchi, Wito wangu kwa wananchi wa Halmashauri zote tatu ni kutoa ushirikiano wa kutosha kwa timu ya wapuliziaji, Viongozi wa kaya mnatakiwa kuhakikisha mnaandaa nyumba zenu kwa tarehe husika ili kuhakikisha nyumba zote stahiki zinapuliziwa dawa ili kuhakikisha tunapata matokeo mazuri na kuendelea kupunguza maambukizi ya malaria kwenye Mkoa wetu.

Ni muhimu mfahamu kwamba shughuli hii inaweza tu kuwa na ufanisi endapo angalu 85% ya nyumba stahiki katika kila eneo tarajiwa zitakuwa zimepuliziwa dawa.

Naagiza viongozi na watendaji wote kuanzia ngazi ya Tarafa, Kata, Kijiji na Kitongoji kusimamia zoezi hili kwenye maeneo yao na kuhakikisha lengo tarajiwa linafikiwa. Ni wajibu wa kila kiongozi na Mtendaji kuhamasisha wananchi wanapatiwa ratiba na kufungua nyumba zao kwa ajiri ya kupulizia dawa ya ukoko.

Aidha, naagiza vyombo na kamati zote za Ulinzi na Usalama katika ngazi zote kushiriki kikamilifu katika zoezi hili na kuwa macho na vitendo vyote vya hujuma kama wizi wa dawa zinazotumiwa kwa matumizi mengine (Pamba n.k). Kuhusu dawa Pamba tumepata dawa chupa 45,000 wiki hii kwa ajiri ya kupulizia mashamba ya Pamba.

Ndugu Wananchi, Mwisho niwaombe tena kutoa ushirikiano mkubwa katika utekelezaji wa zoezi hili muhimu ili kupambana na malaria katika Mkoa wetu wa Mwanza. Napenda kuisitiza kuwa zoezi hili litaanza tarehe 14/02/2018 katika Halmashauri zote tatu. Mimi pamoja na watendaji wenzangu na watendaji kutoka ngazi ya Mkoa tutafuatilia kwa karibu sana kuhakikisha zoezi hili linafanikiwa kwa aslimia 100. Vilevile napenda kuwashukru watu na Serikali ya Marekani, kwa msaada wao mkubwa katika kufadhili mpango huu muhimu sana wa afya kwa umma.

Nina matumaini makubwa kuwa kwa pamoja, tunaweza kushinda vita dhidi ya malaria.

MWANZA BILA MALARIA INAWEZEKANA
"MALARIA HAIKUBALIKI"

ASANTE SANA

Imetolewa na:



Mh: Emmanuel E. Kipole

MKUU WA WILAYA
SENGEREMA

MKUU WA WILAYA
SENGEREMA